

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 10 Aprili, 2012

(Mkutano Ullanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

SPIKA: Naomba tuendelee kusimama, tumkumbuke msanii maarufu wa nchi yetu, Marehemu Steven Charles Kanumba, ambaye kipindi fulani mwaka jana alikuja tukamtambulisha hapa na wenzake, lakini Mwenyezi Mungu amechukua roho yake. Naomba tumkumbuke kwa muda wa dakika moja.

(Hapa Wabunge walismama kwa dakika moja kumkumbuka Marehemu Steven Charles Kanumba)

KIAPO CHA UTII

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, naona wanaotakiwa kuapishwa hawapo na kwa mujibu wa Kanuni zetu, kazi ya kwanza ya Kikao cha Bunge ni kuwaapisha Wabunge wapya; sasa kama hawapo mimi sina sababu na kwa hiyo itabidi waapishwe siku ambayo Kamati ya Uongozi itaipanga. Wataapishwa siku ambayo Kamati ya Uongozi itapanga kwa sababu kazi za humu ndani zinaongozwa kwa mujibu wa taratibu zetu na Kamati ya Uongozi ndiyo inayopanga na ndiyo iliyopanga kwamba kwanza tunawaapisha halafu tunaendelea na shughuli nyingine.

Kwa hiyo, Kamati ya Uongozi ndiyo itapanga ni lini hawa waapishwe. Katibu, tuendelee na hatua inayofuata.

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Sita wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ya Serikali iitwayo *The Anti Money Laundering (Amendment) Bill, 2012* na *The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2012*, kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba, Miswada hiyo imekwishapata Kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa sheria za nchi zinazoitwa *The Anti Money Laundering (Amendment) Act, 2012 No. 1* ya Mwaka 2012 na *The Constitutional Review (Amendment) Act 2012 No. 2* ya Mwaka 2012.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tumekuwa na Sheria hizi mbili tayari zimeshakubalika, tunapenda kumshukuru Rais, kwa kufanya haraka kusaini Miswada hii. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu. Nani atamwulizia swali hilo? Mheshimiwa Diana Chilolo utamwulizia kwa niaba yake.

Na. 1

Wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Wilaya

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y.) MHE. MWIGULU L. N. MADELU
aliuliza:-

Serikali ilibadilisha aina ya Wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Wilaya kwa kuwaondoa Madiwani na kuweka Wataalam:-

- (a) Je, ni nini faida na hasara za mabadiliko hayo?
- (b) Je, kwa nini Serikali haichukui hatua dhidi ya Wataalam wasio waaminifu ambao wametengeneza kampuni zao binafsi kinyume na Kanuni za Utumishi zinazowakataza kufanya biashara ndani ya Ofisi za Umma?
- (c) Je, Serikali haioni kuwa ni vyema wakawarudisha Madiwani kwenye Bodi za Zabuni za Wilaya ili waweze kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Miradi na thamani ya fedha ya Mradi husika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mcemba, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mujibu wa sheria zilizopo, Madiwani siyo Wajumbe wa Bodi ya Zabuni za Halmashauri. Madiwani wanalo jukumu la kusimamia sheria, kutoa maamuzi na kusimamia Halmashauri kwa mujibu wa sheria, taratibu na miongozo iliyopo. Aidha, wataalam katika Bodi za Zabuni kazi yao ni kulishauri Baraza la Madiwani ili lifikie maamuzi sahihi. Hivyo, kuingiza Madiwani katika Bodi za Zabuni ni kulifanya Baraza hilo kushindwa kusimamia na kulinda maslahi ya Halmashauri kama chombo cha maamuzi ndani ya Halmashauri. Faida zinazotokana na kuwatumbua wataalamu katika Bodi za zabuni ni kubwa hasa ikizingatiwa kuwa asilimia kubwa ya fedha za umma katika Halmashauri zinapitia katika Kitengo cha Manunuzi na hivyo kuhitaji ushauri wa kitaalamu ili maamuzi sahihi yafanyike kwa mujibu wa sheria. Kimsingi, hakuna hasara zinazotokana na kuwatumbua wataalam katika Bodi za Zabuni na inapotokea watendaji kukiuka sheria na taratibu za manunuzi, hatua za kisheria huchukuliwa dhidi yao kwa mujibu wa sheria zilizopo.

(b) Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 6 (1) – (8) ya Tangazo la Serikali Na. 177 kuhusu Bodi za Zabuni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa la Mwaka 2007, linawataka Maafisa wa Halmashauri, Madiwani na Wajumbe wa Bodi za Zabuni kutenganisha maslahi binafsi na mchakato wa zabuni katika Halmashauri kuwa waadilifu na kuepuka vitendo vya rushwa na upendeleo katika zabuni. Aidha, Halmashauri haziruhusiwi kufanya manunuzi kutoka kwa kampuni inayomilikiwa na mtumishi wa Halmashauri hiyo. Serikali haitasita kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Mtumishi ye yeyote wa Serikali kukiuka sheria, taratibu na kanuni za ununuzi wa vifaa na huduma Serikalini.

(c) Mheshimiwa Spika, majukumu ya Madiwani yameainishwa katika Kanuni ya 17 ya Tangazo la Serikali Na.177 la Mwaka 2007 kwamba Madiwani wanatakiwa kusimamia kwa Karibu mchakato mzima wa manunuzi katika Halmashauri zao. Hivyo, Madiwani wataendelea kusimamia utekekezaji wa Sheria na Kanuni za Manunuzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuhakikisha zinazingatiwa ipasavyo.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nilitaka kujua kwa sababu hizi tetesi zimeenea

sana za Watumishi wasio waaminifu kupitisha Mradi ama kujipitishia *tender* wakiwa na asilimia kwenye kampuni iliyopata *tender* ama wakiwa kwa kiwango fulani ni wamiliki:

(i) Je, Serikali katika kufuatilia kwa kutumia vyombo vyake ni katika maeneo yapi imeweza kugundua hili?

(ii) Madiwani walipokuwa sehemu ya *Tender Board* walikuwa wakifuatilia hatua kwa hatua fedha zilizotengwa na *value for money*. Nilitaka kujua kati ya kipindi kilichopita na kipindi cha sasa ni kipi ufanisi umekuwa mkubwa zaidi? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niiweke vizuri hapa; jambo linalozungumzwa hapa ni kubwa sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Mchomba kwa kulileta jambo hili hapa. Asilimia 75 ya mapato yote ya Serikali kwa maana ya Halmashauri yanapita katika ...

SPIKA: Tumia *microphone*.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, nitatumia *mic* na nitakuangalia wewe maana ni jambo gumu. Kama anatuambia katika Bunge hili kwamba kuna Mtumishi au kuna Watumishi na tetesi zinatoka, sisi tunachoomba kwanza kabisa atupatie majina ya Watumishi hao. Kwa niaba ya Waziri Mkuu, sisi tutachukua hatua zinazotakiwa.

Suala la kwamba tumeanya uchunguzi na kuangalia kama kuna watu ambao wamefanya hivyo, hilo siwezi kulisema hapa kwa sababu hakuna matukio ambayo nimeyapata; lakini ninajua kwamba katika Halmashauri ya Dodoma, pamewahi kutokea msukosuko hapa mpaka tukawasimamisha watumishi pale kupitia jambo hili ambalo Mheshimiwa Nchemba analizungumzia hapa na tumekuwa tunachukua hatua mbalimbali katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, anauliza kwenye kipengele (b) kwamba tukilinganisha wakati ule tulipokuwa tunawatumia Madiwani na sasa ambapo hatuwatumii tena ni wakati gani ambapo tunaona tumefanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mustapha Mkullo, alikuja hapa na Sheria hii ya Manunuzi iliyosema kupitia kwake na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wataunda Kanuni

ambazo zitasimamia jambo hili. Kwa sasa tunapozungumza hapa hawawezi kukutana kwenye Halmashauri wakaamua pale halafu wakamaliza wakaenda moja kwa moja kwenye *field* kufanya kazi, zitaundwa kanuni ambazo zitatikiwa kupelekwa kwenye Kamati ya Mipango, Uchumi na Uongozi katika Halmashauri. Majina huwa yanatofautiana katil ya Halmashauri, Manispaa na Halmashauri za kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kinachozungumzwa hapa ni kwamba, kwa hivi sasa haiwezekani, Bodi ile ikikaa ni lazima itapeleka pale na kwenye ile Kamati, kama watafika mahali hawakuridhika na mwenendo mzima wa maamuzi yaliyofanyika pale, watakwenda kwenye *regulatory* ndiyo wataofanya maamuzi yale. Kwa hiyo, sioni wasiwasi kabisa katika jambo hili, nina hakika tunakwenda nalo vizuri na ninataka nilithibitishie Bunge hili kwamba tutalisimamia. Ninawaomba kama kuna majina mnayafahamu tuleteeni.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri au Mheshimiwa Meya ndiye ambaye huwa anasaini *tender* ambayo imepitishwa na Kamati ya Bodi ya Watendaji; na kwa kuwa ndani ya Bodi hakuna mwakilishi yejote wa Mstahiki Meya au Mwenyekiti kwa maana ya Diwani; je, Serikali haionti kwamba Mwenyekiti ama Meya kusaini *tender* iliyopitishwa na watu wengine ni kutokumtendea haki? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka niungane na majibu ya Naibu Waziri kwamba hapa lipo suala la utendaji na la usimamizi; Watendaji ndiyo wanakaa katika *Tender Board*. Juzi hapa katika Kikao cha Bunge kilichopita, hoja hii ilitoka kwamba inakuwaje Meya, Mwenyekiti wa Halmashauri, anaambiwa saini hapa mkataba, tukafanya marekebisho kwamba wataalam wakishakaa wakishafanya mapendekezo nani ameshinda hiyo *tender*, Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri atashauriwa na Kamati ya Fedha. Kwa maana hiyo, hakuna mkataba wowote utakaosainiwa Halmashauri na huyo aliye-*tender* bila idhini ya Kamati ya fedha. Kamati ya Fedha ndiyo itakayomshauri Mstahiki Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala la ushiriki wa Madiwani hapo lipo dhahiri, lakini la msingi ni kwamba tumewaondoa Madiwani wawe wameshika hatamu tusiwapeleke jikoni kupika. (*Makofii*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwanza, tukubaliane kwamba jambo hili limekuwa gumu na hao watendaji ambao wanaingia kwenye hiyo Bodi hata mara moja hawajafanya vizuri sana. Sasa kama ukweli ndiyo huo na wameachiwa nafasi hiyo ya kushiriki kwenye Bodi na baadaye walete huku kwa ajili ya Mwenyekiti kusaini kwanza, inasababisha katika mazingira mengine ucheleweshaji maana Mwenyekiti akiona kuna walakini anaweza asisaini, kwa hiyo, kunakuwa na mivutano ambayo inapelekea ufanisi kutokuwa mzuri.

Mheshimiwa Spika, swalii langu ni kwamba; Waziri haoni haja ya kufanya uchunguzi wa jambo hili kuliko kuwa na msimamo huo? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi, hawezi kuwa na msimamo tofauti na Bunge; msimamo wa Bunge unasema tangazo la *tender* litatoka wataomba, wataalam watachambua na watamshauri Mwenyekiti wa Halmashauri asaini ule mkataba. Mwenyekiti wa Halmashauri kabla hajasaini ule mkataba, Bunge hapa ndani tuliamua nani anamshauri Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri kukataa au kusaini tukasema ni Kamati ya Fedha kwa niaba ya Madiwani. Kwa hiyo, Waziri wa Nchi hawezi kuwa na msimamo tofauti na Bunge. (*Makofii*)

Na. 2

Ukamilishaji wa Barabara ya Phantom – MWAMUA

MHE. JAMES D. LEMBELI aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Uchaguzi 2005, Mheshimiwa Rais aliahidi kuwa Serikali itajenga walau barabara moja ya lami katika Mji wa Kahama ambayo inatoka Phantom hadi Mwamua yenyeye urefu wa karibu kilomita tano na kwa mwaka 2006 - 2010 Serikali ilitekeleza ahadi hiyo kwa asilimia 50:-

- (a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa eneo hilo kuhusu kukamilisha sehemu iliyobaki?
- (b) Je, Serikali imewachukulia hatua gani za kisheria waliojenga kipande cha awali cha barabara hiyo ambayo ilikuwa chini ya kiwango na kusababisha kuchakaa kwa barabara hiyo muda mfupi baada ya kujengwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa James Daud Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Rais alitoa ahadi ya kujenga barabara kutoka Phantom hadi Mwamua, sawa na kilomita tano kwa kiwango cha lami. Serikali kwa kuzingatia ahadi ya Rais ilianza utekelezaji wa Mradi huo kwa awamu ambapo mwaka 2009/2010 zilijengwa kilomita 1.5 kwa kiwango cha lami, kilichogharimu shilingi milioni 527.3. Katika mwaka wa Fedha wa 2010/2011, kilomita nyingine 1.7 zilijengwa kwa gharama ya shilingi milioni 547.9 kwa kiwango cha lami. Kazi ya ujenzi wa barabara hiyo inaendelea ambapo mpango wa mwaka 2011/2012 ni kujenga kilomita 1.2 kwa gharama ya shilingi milioni 535.4. Kazi itaendelea hadi zitakapokamilika kujengwa kilomita tano zilizoahidiwa na Rais.

(b) Mheshimiwa Spika, kuharibika kwa kipande cha awali cha barabara hiyo kulitokana na kiwango hafifu cha ushindiliaji (*poor compaction*) na hivyo kusababisha maji kupenya chini ya barabara na kuifanya iharibike. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kumwamuru Mkandarasi ambaye ni *Jasco Construction Co. Ltd.*, kurudia matengenezo ya barabara hiyo katika sehemu zote zilizoharibika kwa gharama zake. Mkandarasi huyo yupo katika eneo la Mradi na anaendelea kurekebisha upungufu uliojitokeza.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yanatia wasiwasi kwamba ahadi hii ya Rais itatekelezwa kama alivyodhamiria na kwa kipindi alichotaka, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa kuwa kwa mujibu wa majibu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilipanga kujenga awamu ya tatu ya ujenzi wa barabara hiyo, na kwa kuwa zimebakia miezi mitatu na kazi haijaanza: Waziri anawaambia wananchi wa Mji wa Kahama kwamba kazi hiyo itaanza lini?
- (b) Wakandarasi kama Jasco ambao kazi zao kimsingi zimekuwa hafifu na wanafanya kazi maeneo mengi ya Wilaya ya Kahama, Serikali inawachukulia hatua gani ili wasiendelee kuchezea fedha za Serikali? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hapa tumetoka kwenye sherehe za Pasaka, na moja ya mambo ambayo tumejifunza ni kutokuwa kama Tomaso ambaye hakuamini kwamba Bwana Yesu amefufuka. Nataka nimthibitishie ndugu yangu na rafiki yangu Mheshimia James Daudi Lembeli kwamba jambo hili wala asiwe na wasiwasi nalo wala asiwe na hofu nalo.

Nimeeleza hapa zilivyolipwa na hizi zinazozungumzwa hapa, wala sio kwamba nimezungumza kwamba napata jibu tu nakuja nalo. Hivi Rais alipokwenda kule Kahama, alipotoa ahadi ile, ujue jinsi ambavyo jambo hili lilichukuliwa kwa uzito wala hela hazikutoka kwenye Halmashauri. Hela zimetoka katika Mfuko wa Barabara ambao unasimamiwa na Wizara ya Ujenzi, na maelekezo yakatolewa kupitia Mfuko wa Barabara kwamba hela zinazotakiwa kwa ajili ya hii barabara inayozungumzwa hapa ambazo katika hali ya kawaida zingetoka katika Halmashauri, ndiyo hii niliyoisoma hapa.

Sasa anasema, kuhusu awamu ya tatu ambayo nimeisema hapa, mimi nataka nimthibitishie na nataka nimwambie Mheshimiwa Lembeli kwamba, tunaendelea kuwasiliana na wenzetu walioko katika Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROAD* kuhakikisha kwamba hela zinapatikana hapa. Mheshimiwa Rais amekwishatoa tamko kwamba hii barabara ijengwe na sisi tutasimamia kuhakikisha kwamba inajengwa.

Sasa la pili amezungumza kuhusu suala la wakandarasi ambao wanafanya kazi ambazo siyo nzuri na nini, na matokeo yake tumpata ya kwamba wamerudishwa kule wanakofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, umetuona kila siku tunatembea na *tape measure* barabarani. Nataka niseme hapa na niwaambie Watanzania kwamba tuko *serious*. Kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukimkuta Mkandarasi amefanya kazi ya hovsky, tunasimamisha kazi ile mara moja pale pale, na tunamwambia ondoka. Kama anakwenda Mahakamani, tunamwambia atangulie kule, halafu sisi tutakutana naye huko huko Mahakamani. Kwa hiyo, nataka kusema kabisa tuelewane hapa kwamba, Jasco tumemwambia arudi akafanye kazi ile katika kiwango kilichozungumzwa katika mkataba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sauti hii unaifahamu toka tulipoingia katika Bunge hili, huwa ni kubwa. Ni msisitizo tu mimi nafanya hapa. Lakini nataka niseme hatumwachi Mkandarasi ye yeyote atakayetuvurugia kazi katika Halmashauri. Hatutamwachia kabisa! Kwa hiyo, hili jambo linaloendelea hapa tumemwambia mkandarasi yule afanye kazi. Mheshimiwa Lembeli kama ana wasiwasi tukimaliza Bunge hapa,

tupande ndege, tuondoke wote twende mpaka Kahama tukaangalie hiyo habari tunayozungumza hapa. (*Makofii*)

SPIKA: Sasa sijui Tomaso ni Mheshimiwa James Lembeli au nani? Umetuacha hoi hapa, sijui nani Tomaso sasa! Hili swali ni maalum. Swali linalofuata Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Na. 3

Vigezo Vinavyotumika Kupanga Mishahara ya Watumishi wa Umma

MHE. MOSES J. MACHALI aliuliza:-

- (a) Je, Serikali inatumia vigezo gani kutofautisha mishahara ya kada mbalimbali za watumishi wa umma kama vile Walimu, Madaktari; kwa mfano, Mwalimu mwenye shahada analipwa Sh. 400,000/= lakini Daktari mwenye shahada analipwa Sh. 900,000/= wanapoanza kazi?
- (b) Je, hali ya namna hiyo siyo ubaguzi na kwamba inawavunja moyo baadhi ya watumishi wale walio na viwango vyta elimu sawa, lakini wanalipwa kidogo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mwalimu mwenye shahada huanza na mshahara wa Sh. 469,200/= kwa mwezi na mshahara wa Daktari mwenye shahada huanzia Sh. 975,700/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Machali lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tofauti ya viwango vyta mshahara kati ya kada moja na nyingine inatokana na uzito wa majukumu uliofikiwa baada ya tathmini ya kazi ambayo hufanyika ili kubaini uzito wa majukumu kwa kila kada. Uzito wa kazi hupimwa kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

- Kiwango cha elimu na muda unaohitajika kupata elimu hiyo;

- Uzoefu unaohitajika kufanya kazi husika;
- Usimamizi wa rasilimali kama vile fedha, vifaa na rasilimali watu;
- Athari, au umuhimu wa kazi husika kwa jamii;
- Mazingira ya kazi na uhuru wa kufanya maamuzi wakati wa kutekeleza jukumu husika.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu hutumika hata katika sekta binafsi na duniani kote na ndiyo unaotumika katika Utumishi wa Umma kupima tofauti ya majukumu mionganoni mwa kada zilizopo katika utumishi wa umma. Hata hivyo, uzito wa majukumu mionganoni mwa kada ndio msingi wa kutofautiana kwa viwango vyatia mishahara.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya kazi iliyofanyika Serikalini mwaka 2000 inaonyesha kuwa kada ya Uduktari ilikuwa na uzito mkubwa ikilinganishwa na kada nyingine na ndivyo maana ikatengewa mshahara mkubwa ikilinganishwa na kada nyingine. Pamoja na kwamba viwango vyatia elimu mionganoni mwa watumishi wa kada mbalimbali vinaweza kufanana, ni ukweli usiopingika kwamba uzito wa majukumu hauwezi ukalingana kwa kada zote. Kwa mfano, uzito wa kazi ya kwamba Daktari hauwezi kuwa sawa na uzito wa kazi ya Afisa Utumishi pamoja na ukweli kwamba wote ni wahitimu wenye shahada ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna ubaguzi katika kupanga mishahara ya watumishi wa umma. (*Makof*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili kusudi niweze kumwuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

- (a) Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri, ametueleza kwamba tathmini iliyofanywa mwaka 2000 inaonekana kwamba kada ya Uduktari inaonekana kuwa na majukumu makubwa kuliko kada nyingine. Nilikuwa naomba anisaidie kuweza kujua kada ya pili kwa kuwa na majukumu mazito ni kada gani katika kada hizo za watumishi mbalimbali?
- (b) Binafsi ninaona sina imani na tathmini iliyoweza kufanyika kuhusiana na kada mbalimbali za watumishi ikiambatana pamoja na majukumu yao. Naamini kuna haja ya kuweza kuangalia kada ya watumishi kama vile Walimu. Walimu wana

majukumu makubwa sana na mishahara yao ni kidogo. Kwa mfano,...

SPIKA: Inabidi uulize swali, siyo hotuba.

MHE. MOSES J. MACHALI: Hivyo basi, kwa mfano ukijaribu kuangalia tofauti ya mshahara wa Daktari mwenye shahada na Mwalimu mwenye shahada ni takribani Sh. 488,500/=. Tofauti hii ni kubwa sana. Naomba Waziri wa Utumishi kutoka Ofisi ya Rais atusaidie kujua ni lini Serikali itaweza angalau kuweza kuhakikisha kwamba inaboresha mishahara ya watumishi kama Walimu, Polisi, Mahakimu ili *gape* lisiwe kubwa kama ambavyo inaonekana hivi sasa kwa sababu hizi kada nyingine wanalamika na wanaonewa kweli kweli. Naomba Waziri aweze kutuambia ni lini mishahara hii itaweza kuboreshwa hasa ya Walimu, Polisi na Mahakimu. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, kwanza, Mheshimiwa Machali alipenda kufahamu kada nyingine ambazo zilionekana kuwa na uzito mkubwa wakati wa kufanya tathmini. Ni Wanasheria na Wahandisi ndio amba walifuatia baada ya Madaktari.

Suala lingine ambalo alitaka kufahamu alisema kwamba hana imani na tathmini iliyotumika. Kama nilivyojibu kwamba, hivyo ni vigezo vya kimataifa na vinatumika kila mahali. Kwa sababu Mwalimu na Daktari ni kweli wote wana majukumu makubwa. Lakini hata kwa kuangalia muda waliotumia katika kupata shahada zao za kwanza, Mwalimu anatumia miaka mitatu, baadhi yao; lakini Daktari, wengine ni zaidi ya miaka mitano. Siyo chini ya miaka mitano Daktari anapata elimu yake. Kwa hiyo, pamoja na kwamba wote mna *degree* za kwanza, lakini huwezi kumlinganisha mtu aliyechukua *degree* yake kwa miaka mitatu na aliyechukua *degree* yake kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, pia, tunaangalia hali ya mazingira ambayo mtu anafanya kazi kiakili na hata yale mazingira yake. Kwa kumwangalia Daktari, anafanya kazi katika mazingira magumu zaidi kuliko hata Mwalimu. Ni wangapi kati yetu sisi hapa unaweza kwenda kumhudumia labda maiti au mtu aliyelemta ajali wewe mwenyewe? Kwa hiyo, ni vitu vyote hivyo ambavyo vinaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwamba, ni lini Serikali itahakikisha kwamba inaboresha mishahara ya watumishi? Ni kwamba kadri uchumi unavyokua, mishahara ya watumishi inaboresha. Lakini ili kupunguza hili *gap* ambayo ipo katika utumishi wa umma, tumepitisha

sera ya mishahara na motisha katika utumishi wa umma, na sasa hivi tayari Bodi imeshaundwa na Mwenyekiti na mtendaji mkuu wa hiyo bodi tayari wameshateuliwa. Lengo ni kuhakikisha kwamba ndani ya utumishi wa umma tunafanya tathmini ya kazi kwa watumishi wote na kwamba tunawianisha mishahara ya watumishi wa umma, ndani ya utumishi wa umma na katika Taasisi kuhakikisha kwamba tunapunguza *gap* kuliko ambavyo ipo sasa hivi.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala zima la mishahara hasa wafanyakazi wa kada ya chini imekuwa ni tatizo kubwa sana katika suala zima la *purchasing power* na tumeona wazi kwamba hata Serikali inapoongeza mishahara wanufaika zaidi ni wale Maafisa na watu katika ngazi mbalimbali katika Idara za juu: Je, Serikali imejipanga vipi katika mwaka huu wa fedha kuhakikisha kwamba mishahara hata ikiwa na ongezeko, wanakaoguswa zaidi ni watu wa kada ya chini badala ya kuangalia utaratibu wa *flat rate*?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, tunavyopanga mishahara na kuangalia kada mbalimbali na watumishi wa ngazi mbalimbali, pia tunaangalia na sekta binafsi ndani ya soko la ajira wengine wanalipa nini. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunawabakiza watumishi katika utumishi wa umma. Kuhusu kupanga, kwamba tunapanga *flat rate*, siyo kweli kwamba tunapanga *flat rate*, tunapanga kwa kuzingatia vigezo ambavyo nimevielezea katika suala la msingi.

Na. 4

Athari za Mgomo wa Madaktari

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA aliuliza:-

- (a) Je, mgomo wa Madaktari umeathiri vipi jamii ya Watanzania?
- (b) Je, ni watu wangapi walikufa kwa kukosa huduma wakati wa mgomo huo?
- (c) Je, ni maeneo gani ya nchi yetu yaliathirika sana na mgomo huo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

(a) Mgomo wa Madaktari ulitokea kwa awamu mbili katika Hospitali za Serikali, umeathiri Watanzania kisaikolojia kwa namna tofauti kutokana na kuwa kuna baadhi ya wagonjwa walikuwa wanaumwa na walikosa huduma kwenye maeneo ya hospitali walizotarajia. Vile vile wapo Watanzania walioathirika kutokana na masikitiko ya kuona Watanzania wenzao wakikosa huduma za afya kutokana na mgomo wa madaktari. Athari nyingine ni ya kiuchumi ambapo baadhi ya wagonjwa ilibidi wapate huduma za malipo kupitia Hospitali za watu binafsi.

Pia kuna watumishi wa afya waliokuwa wakiendelea na kazi wakati wa mgomo ambao walipata usumbufu mkubwa kutoka kwa waendesha mgomo kwa kushinikizwa wajunge na mgomo pamoja na kutishiwa usalama wao. Wizara yangu imesikitishwa na mgomo huo na inatoa pole kwa wale wote walioathirika kwa namna moja au nyingine.

Hospitali nyingi zilizokumbwa na mgomo huo zimetoa taarifa kuwa hakukuwa na ongezeko la vifo ambavyo vinahusishwa moja kwa moja na mgomo. Kwa mfano, takwimu za vifo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili zimelinganishwa kama ifuatavyo:

Kabla ya mgomo mwezi Novemba, kulikuwa na vifo 457, mwezi Desemba kulikuwa na vifo 537 na wakati wa mgomo mwezi Januari, kulikuwa na vifo 475 na wiki ya kwanza ya mwezi Februari, kulikuwa na vifo 95.

(b) Mgomo wa madaktari ulitokea katika hospitali 13 ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali tatu za Manispaa za Dar es Salaam; Amana, Temeke na Mwanyamala; Taasisi ya Kansa ya *Ocean Road*; Hospitali za Rufaa - Bugando, Mbeya na KCMC. Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Tanga, Morogoro, Dodoma, Arusha na Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili. Maeneo yaliyoathirika sana ni Hospitali ya Taifa na Hospitali tatu za Manispaa za Dar es Salaam. Nikzungumzia Hospitali ya Taifa, maana yake ni kwamba na Taasisi ya Mifupa ya MOI imo ndani yake.

Mheshimiwa Spika, Hospitali za Manispaa za Dar es Salaam zilizoathirika ni Amana, Temeke na Mwanyamala.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niseme nimeshtuka sana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo kwa tasfiri ya kawaida tu nimepata sura ya kuwa kumbe huu mgomo haukuleta vifo kwa Watanzania. Sasa kama hivyo ndivyo, kwa nini imetolewa ulinganisho wa Hospitali moja tu ya Muhimbili na kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri Hospitali 13 zilikumbwa na mkasa huu?

- (a) Kwa nini ulinganisho wa vifo umetolewa kwa hospitali moja tu ya Muhimbili?
- (b) Mimi nina imani kuwa watu wamekufa kwa sababu kijana wangu amekufa katika mgomo huu. Sasa ukiniambia hakuna ongezeko la vifo, napata taabu kuamini. Sasa naiuliza Serikali: Je, inawapoozaje machozi wale waliopatwa na vifo vya watu wao katika mgomo huo? Kwa sababu ikiwa mtu aliyemchoma mtu kisu barabarani anahukumiwa kuua, Daktari anagoma, inakuwa kimya tu hivi hivi; na panatolewa majibu kuwa hapakuwa na vifo: Hii hali, tunakwenda wapi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwenye jibu langu la msingi nimemwelezea Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kwamba vifo ambavyo vimetokea katika Hospitali hizi huwezi ukasema kwamba vinahusishwa na mgomo moja kwa moja, kwa sababu ukiangalia takwimu za hospitali ambayo imeathirika sana ambayo ni Muhimbili, ni kwamba kulikuwa hakuna tofauti kubwa, na hizi ni takwimu ambazo nimezifuata *Mortuary*, wala sikuuliza Watendaji wanilettee. Nimekwenda *Mortuary* nikaangalia zile *records* ambazo zilikuwepo mwezi mmoja kabla na ule mwezi ambao kulikuwa na mgomo.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tumefanya ulinganisho wa Muhimbili? Tumefanya ulinganisho wa Muhimbili kwa sababu katika maeneo mengine, mgomo uliotokea haukupita siku mbili, zaidi ya masaa 24, lakini Muhimbili walianza kugoma ma-*intern* wakaja wakaendelea kwa siku mbili wakagoma mabingwa. Sasa hapo ndiyo tuliona kwamba ingegusa sana afya za Watanzania waliokuwa wamelazwa katika hospitali ya Muhimbili. Ndiyo sababu niliona kwamba kwa sababu ni Hospitali ya Taifa, na mgomo ule ulikuja ukagusa mabingwa ambako maeneo mengine kwa mfano Hospitali ya Dodoma na hizo Hospitali nyingine zote za Mikoa waligoma kwa masaa, na baada ya pale, mabingwa wote walikuwa wanaendelea kufanya kazi.

Pale ambako mabingwa na manesi wanafanya kazi, naomba niseme kwamba huduma ziliboreshwu na kwamba ndiyo kipindi pekee ambacho

tuliona kwamba mabingwa wanaingia wodini na wanafanya kazi badala ya kutegemea wale madakatri ambao walikuwa kwenye mafunzo. Mojawapo ya kusema kwamba kwa nini huduma ziliboreka ni hizo. Lakini vinginevyo, wale madaktari ambao waligoma tukasema kwamba tuwachukulie hatua, utamchukulia hatua kwa namna gani ambavyo mgonjwa alikuwa amelazwa na alikuwa ni mgonjwa na anaendelea kupewa dawa kwa bahati mbaya kafariki kwenye kiwango kile kile ambacho watu wanafariki pale Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, inabidi tufanye utafiti ambao unaitwa ni *verbal autopsy*, utahitaji pesa tuweze kuchambua, tuone kwamba ni yupi kweli alikuwa amekufa kutokana na maradhi yake na yupi ambaye amekufa kwa sababu hakupata huduma ya wale madaktari, *junior doctors* ambao waligoma.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kuniona niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mionganoni mwa sababu zilizosababisha madaktari wagome ni pamoja na ukosefu wa vitendea kazi mfano *gloves*, mashine zile zilikuwa hazifanyi kazi za *x-ray*, lakini pia madawa yalikuwa hayapatikani kwa upande ya wagonjwa.

Je, baada ya mgomo huo, Serikali imeshughulikia vipi haya matatizo ili yasijirudie na yakasababisha mgomo mwingine?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba nimjibu Mheshimiwa Paulina Gekul, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Karatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba madaktari waligoma, lakini kuanzia mwanzoni mwa ule mgomo, nilishughulika nao, na madai yao tangu mwanzo yalikuwa ni maslahi. Madai ya kuja kuzungumzia haki za wagonjwa na vitendea kazi yalikuja baada ya kuona wananchi *wana-react* kwa kusema kwamba ninyi mnatuacha tufe kwa sababu ya maslahi yenu, lakini sababu ya msingi ilikuwa ni kwamba kwanza *maintern* wale ambao waligoma Muhimbili wakasema kwamba wameshajaza nafasi tukawapeleka kwagine.

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili illiyofuata baada ya hapo walipo-*hijack* Chama cha Madaktari Tanzania ilikuwa ni maslahi yao, maslahi namba moja ilikuwa ni kwamba wanataka *on call allowance* iongezwe pamoja na kupata nyumba na kupata kadi za matibabu za Bima ya Afya

za kijani, haya mengine hata kama mkiangalia *trend* ya walivyokuwa wanabadilika zile Kamati zao ni kwamba walikuwa wanaangalia ni ipi sasa ambayo itatupa *support*, lakini naomba kusema kwamba Serikali imejitahidi sana, hospitali ya Muhibili ina vitendea kazi, mashine sio binadamu inafika mahali inahitaji matengenezo.

Mheshimiwa Spika, tulikosa *film* hapa katikati kwa sabau dunia nzima *supply* ilikuwa ina matatizo, lakini zimeshafika na dawa zilikuwepo. Pale ambapo hazipo, hospitali zote hata *private* dawa nyingine pia hazipo, wananchi wanashauriwa waende kununua na wale wenye Bima ya Afya wanapata kutokana na Bima ya Afya. Ahsante.

Na. 5

Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Singida

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Mkoa wa Singida upo katika ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ambayo itakuwa na vitengo vyote muhimu na kwamba baadhi ya vitengo vitakamilika hivi karibuni:-

- (a) Je, Serikali iko tayari kushirikiana na uongozi wa Mkoa kuandaa madaktari kwa ajili ya Hospitali hiyo?
- (b) Je, Serikali imetenga shilingi ngapi katika Bajeti ya mwaka 2012 ili kusaidia ujenzi huo unaondelea?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Singida kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Singida ili kuhakikisha kwamba huduma za afya zinatolewa katika hospitali hii pindi itakapokamilika. Uongozi wa Mkoa wa Singida unatakiwa kuwasilisha maombi yao katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili kuwezeshwa kupata watumishi wenye sifa stahiki pamoja na upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa hospitali hii, kwa kuzingatia utaratibu uliopo, kama ilivyo kwa hospitali nyingine za Rufaa za Mikoa.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Singida. Kiasi hiki ni kutoka katika vyanzo vya ndani vya Serikali na ni sehemu ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyoonekana katika ukurasa 221 wa *volume IV* ya Makisio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mkoa wa Singida. Aidha, Wizara yangu inatoa pongezi za dhati kwa Mkoa wa Singida kwa jitihada kubwa na hatua iliyofikia katika ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa juhudzi za Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Daktari Parseko Kone na sekretarieti yake ni kubwa sana mpaka sasa imeshapata vifaa karibu vyote vya Hospitali hii ya Rufaa na imeshapata madaktari wa kutosha kutoka shirika rafiki la huko Amerika, daktari mmoja bingwa ambaye atafanya kazi hapo muda wote na madaktari 20 wamesema watakuwa wanakuwa kufanya kazi wakati wa *winter* kwa maana ya miezi minne kila mwaka.

Je, Serikali haioni kwamba ili vifaa hivi visiharibike na madaktari hawa tuliowapata tuweze kuwatumia, haioni kwamba kuna kila sababu kutuongezea fedha hizi bilioni mbili angalau iwe bilioni nne ili kuongeza kasi ya ujenzi ya hospitali hii kuokoa vile vifaa tulivyovipata?

(ii) Kwa kuwa nia ni hospitali hii kukamilika mapema na kwa kuwa kuna mashirika ya Serikali ambayo husaidia shughuli za ujenzi hata kwa njia ya kuwekeana mkataba na Serikali kwa mfano *NSSF, PSPF, PPF* Serikali haioni kuna haja ya kutumia mashirika haya kama ilivyoofanya kwenye ujenzi wa Chuo Kikuu cha *UDOM* ili hospitali hii iweze kukamilika mapema?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kumjibu Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Singida kama ifuatavyo:-

Kwanza kwa niaba yangu mimi na kwa niaba ya Serikali naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Daktari Parseko Kone kwa juhudzi zake kubwa anazozionyesha katika kuendeleza Mkoa wa Singida sekta ya afya ikiwa ni mojawapo.

(a) Mheshimiwa Spika, mimi nina amini kwamba Serikali katika bajeti ya mwaka huu ningeshauri kwamba na wao pia sasa waweke kwenye bajeti na sisi kama Wizara husika ya kisekta tutahakikisha kwamba tunalismamia hili ili waweze kuongezewa hizo pesa wanazohitaji kwa ajili ya kukamilisha hiyo hospitali. (*Makofii*)

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna mashirika ya Serikali ambayo yakiingia mkataba na Serikali yanaweza yakasaidia kumalizia ile hospitali, mimi naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi jitihada zianze kwenye Mkoa, wakianza kwenye Mkoa wakizungumza nao na wakaja wakatuuliza sisi, basi na sisi tutakubaliana nao kwamba wawasaidie kumalizia na sisi kila mwaka tunapopata pesa tutakuwa tunawalipa. Lakini hili ni *discretion* ya haya mashirika kwamba kama watakubali kweli kutoa hizo pesa, lakini mimi naomba niseme kwamba wakijaribu kutengeneza huo mkakati na sisi kama Wizara hasa kama watakwenda kushauriana na Bima ya Afya ya Taifa sisi tutakuwa nyuma yao kuhakikisha kwamba tunawadhamani.

Na.6

Ujenzi wa Reli Makambako – Songea - Mbinga na Songea – Tunduru - Mtwara

MHE. JENISTA J. MHAGAMA (k.n.y. MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO) aliuliza:-

Usafiri wa reli ni gharama nafuu na huchukua mizigo mingi zaidi. Je ni lini Serikali itajenga reli kutoka Makambako – Songea - Mbinga na Songea – Tunduru – Mtwara?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba usafiri wa reli ni wa bei nafuu na wenyewe uwezo mkubwa wa kuchukua mizigo mizito na kwa wingi kwa wakati mmoja ukilinganishwa na usafiri wa barabara, pia barabara tutaweza kuziongezea uhai tukitumia reli.

Kama sehemu ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano (2011/2012- 2015/2016), Serikali inatarajia kufanya upembusi yakinifu wa ujenzi wa reli ya kutoka Mtwara – Songea -

Mbamba Bay yenye matawi ya kwenda katika machimbo ya makaa ya mawe na chuma mtawalia yaani kwa pamoja yanayotegemewa kujengwa maeneo ya Mchuchuma na Liganga. Ujenzi wa reli hii ni sehemu ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa uendelezaji wa Ukanda wa Maendeleo ya Mtwara (*Mtwara Development Corridor*).

Aidha, Serikali itaendelea kutafakari mpango wa kujenga reli ya kutoka Makamabako – Songea - Mbanga na Songea – Tunduru - Mtwara hususan baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli ya kutoka Mtwara – Songea - *Mbamba Bay*.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa anapozungumzia mradi wa *Mtwara Corridor* anazungumzia maeneo hayo hayo ya Mtwara, Lindi, Ruvuma kwa maana ya Songea mpaka *Mbamba Bay*. Unapokuwa kule *Mbamba Bay* sasa hivi katika maeneo ya Luanda, eneo la Mgaka makaa ya mawe yameshaanza tayari kuchimbwa na ni karibu sana na Bandari ya *Mbamba Bay*.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba ni busara tu ya hali ya juu kuanza kutengeneza *branch* ama tawi la reli hiyo kutoka pale *Mbamba Bay* kwenda Mgaka na akafikiria hilo tawi lingine la kwenda huko Mchuchuma kwa sababu maeneo haya yote ni *Mtwara Corridor* naomba anipe majibu ya kuzingatia hoja hiyo ya msingi ya kupeleka reli pale Mgaka.

(ii) Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, majibu haya ya upembuzi yakinifu, makakati yamekuwa ni majibu ya kila siku na mipango hiyo mkakati na upembuzi yakinifu umekuwa ukichukua miaka na miaka, sasa kwa kuwa hapa katika majibu ya msingi amesema ni mpango wa maendeleo wa miaka mitano.

Je, anawaambia nini wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na ni lini upembuzi huo haswa sasa utaanza na mradi huo uweze kuanza kwa maendeleo ya wananchi wa Majimbo yote ya Mkoa wa Ruvuma?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi napenda nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge.

Kwanza suala la Mkaga mpaka Bandari ya *Mbamba Bay*, hilo linafanyiwa kazi, kweli ni jirani lakini tunakwenda kwa utaratibu ambao hivi sasa umeandaliwa kitaalamu. Lakini pia kwenye suala la pili la upembuzi yakinifu, hii miaka mitano nitaarifu tu ni kwamba kuna mwekezaji sasa hivi ambaye shughuli zinaratibiwa na Wizara ya Viwanda, Biasara na Masoko na huyu mwekezaji tayari yupo katika maeneo hayo kwa hiyo, tunashirikiana na Wizara ya Uchukuzi ili shughuli hii iendelee, lakini tayari imekwishaanza na tusubiri matokeo mazuri tu.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kumuuliza Mheshimiwa Waziri pamoja na majawabu yake mazuri na nia njema hiyo ya kutaka kujenga reli hiyo, nilitaka tu kuuliza swali dogo, hivi nani anaweza akamuamini sasa ama akatuamini wakati tunayo reli ya kati ya kutoka Kigoma - Mpanda - Kigoma- Mwanza reli hii toka mwaka 1906 tumeiacha, imekufa na leo mizigo inatembea kwa wiki mara moja, lakini leo Waziri anakuja hapa kutuambia mipango mikubwa ya kujenga reli mpya wakati ya zamani tumeiacha; ama hatuihitaji reli hii katika uchumi?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali hivi juzi tu imetupatia shilingi bilioni 45 kwa ajili ya uimarishaji wa reli ya kati, reli hii ina umuhimu mkubwa na Serikali ina ufahamu na ndiyo maana tutachukua sehemu ya reli ambayo ipo kati ya Agondi Kitalaka kuja mpaka Tura na hii reli itawekwa reli yenyenzo wa *pound 80 kwa yard* na hii reli itapelekwa kwenye tawi la reli ya kutoka Taliwa mpaka Mpanda kwa sababu pale ina *pound 54 kwa yard* kwa hiyo, hiyo itaimarika, lakini niongeze pia Wizara inafanya mchakato sasa hivi, tumepata wawekezaji wengi na kutumia rasilimali za ndani na baadhi ya wafanyabiashara wa ndani tumeshirikiana nao, tutaboresha mabehewa, tutaboresha *engine* pamoja na reli yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Serukamba asiwe na wasiwasi na pia Bandari ya Kigoma itaimarika pamoja na Bandari ya Dar es Salaam. Bandari na reli ni sehemu kubwa ya uchumi wa Taifa hili na tunatambua hilo na tunatekeleza kila mradi kama bajeti ilivyoleza mwaka 2010/2015.

Ahadi ya Kuchimba Kisima kwa Wakazi wa Karatu

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE aliluiza:-

Serikali kupitia Wizara ya Maji iliahidi kuchimba kisima cha maji safi na salama kwa gharama ya shilingi 50,000,000/= kwa ajili ya wananchi wa Mji wa Karatu kwa barua ya tarehe 16 Julai, 2010 yenye Kumb. Na. FC.30/50/547/3A/73 lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ahadi hiyo isiyotekelvezwa inawafanya wananchi kukosa imani na Serikali yao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani mahsus wa kuhakikisha ahadi hiyo inatekelezwa haraka iwezekanavyo kuwaondolea wananchi adha ya kukosa maji hasa wakati wa kiangazi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali bado inakumbuka ahadi yake ya kuchimba kisima cha maji safi na salama kwa ajili ya wananchi wa Mji wa Karatu. Fedha za utekelezaji wa kazi hiyo zimetengwa kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa ahadi hiyo itatekelezwa mara fedha zitakapopatikana. Pamoja na kutenge fedha, katika utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Serikali imefanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa vitabu vya zabuni kwa ajili ya Mradi wa Maji wa Karatu. Kazi hiyo imekamilika mwezi Machi, 2010. Hivi sasa fedha zinatafutwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri amekiri kuwa fedha hizo zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2011/2012 na kwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara, naomba kunukuu sehemu ya barua yake ya tarehe 16/7/2010 akimwagiza Meneja wa TAVIWASU, Karatu, kuandaa mchanganuo wa fedha kwa ajili ya mradi huo na kwamba mchanganuo huo ufile kabla ya tarehe 30/7/2010 ili atume shilingi milioni 50 kwa kazi hiyo. Sasa mchanganuo ulipelekwa lakini fedha

hizo hazikutumwa. Inaonyesha kwamba, kwa kuwa mwaka 2010 ulikuwa wakati wa uchaguzi mkuu, Serikali imejaribiwa kuingia kuwapa wananchi matumaini yasiyokuwepo. Sasa naomba Waziri awaambie wananchi wa Karatu kazi hiyo inaanza lini na itakamilika lini maana bajeti ya mwaka 2011/2012 bado miezi miwili tu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba ahadi ya Serikali ipo palepale na kwamba fedha hizo ziko kwenye bajeti. Kwa hiyo, mara tu Hazina itakapowasilisha fedha hizi kwenye Wizara yetu ya Maji, tutazipeleka fedha hizo Karatu kwa ajili ya mradi huo.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi naomba kuuliza swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa suala la upembuzi yakinifu na michanganuo ni la kila siku na tatizo la maji liko katika maeneo mengi ya Tanzania Bara, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba Wabunge hawaji tena hapa Bungeni kulalamikia tatizo la maji katika maeneo yao?

SPIKA: Ingekuwa vizuri kweli. Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nikuhakikishie kwamba siyo kwamba Wabunge tunakuja kulalamika habari ya maji, ni kwamba tunataka kujua Serikali inafanya nini. Mnafahamu kabisa kwamba tunayo programu kubwa ya utekelezaji ya miradi ya maji katika nchi nzima na programu hiyo iko katika vipengele mbalimbali. Suala la upembuzi yakinifu ni suala la msingi, ni lazima ufanye upembuzi yakinifu ili kujua maji utayapata wapi, utayapata chini ya ardhi au unayapata kwenye mabwawa au kwenye mito. Kwa hiyo, mipango ipo na ni endelevu na nina uhakika kabisa baada ya muda si mrefu tutaanza kuona matunda yake hasa katika miradi hii ya mijini pamoja na miradi ya vijiji kumi.

Na. 8

Kusuasua kwa mradi wa maji wa Benki ya Dunia – Geita

MHE. MARIA I. HEWA (K.n.y. MHE. LOLESTIA J.M. BUKWIMBA) aliuliza:-

Mradi wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, kwa muda mrefu umekuwa ukusuasua kupeleka maji katika vijiji viliviyokusudiwa vyta Kata za Katoro, Chigunga, Nyachiluluma, Nyamigota na Nyakagomba:-

Je, mradi huo umefikia hatua gani na ni lini utakamilika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Washirika mbalimbali wa Maendeleo, ikiwemo Benki ya Dunia. Utekelezaji wa Programu katika kipindi cha 2007/2008 hadi 2009/2010 ulihusu ujenzi wa miradi ya maji yenye kuleta matokeo ya haraka. Wakati Halmashauri zinajenga miradi ya maji yenye matokeo ya haraka, zoezi la kuajiri Wataalam Washauri kwa ajili ya usanifu wa miradi ya maji ya vijiji 10 katika kila Halmashauri lilikuwa likiendelea. Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilimwajiri Mtaalam Mshauri *COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Ltd* kwa ajili ya kusanifu miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mtaalam Mshauri tayari alikamilisha utafiti wa maeneo ya kuchimba visima na kazi ya uchimbaji wa visima virefu imekamilika katika vijiji vyote 17. Vijiji hivyo ni Katoro (Kata ya Katoro), Chigunga na Kabugoro (Kata ya Chigunga), Chikobe na Chankoronga (Kata ya Nyachiluluma), Inyala (Kata ya Nyamigota), Nyakagomba na Luhuha (Kata ya Nyakagomba), Kakora, Nyamtukuza na Kitongo (Kata ya Kakora), Kharumwa na Ikangala (Kata ya Kharumwa), Izunya (Kata ya Izunya), Nyarubele (Kata ya Nyijundu) na Bukwimba na Kayenze (Kata ya Bukwimba).

Mheshimiwa Spika, hatua inayofuatia sasa ni ujenzi wa miundombinu ya maji. Wizara yangu illitoa kibali cha kutangaza zabuni za ujenzi wa miundombinu katika vijiji vya Nyamtukuza, Luhuha na Nyakagomba na kufunga pampu za maji katika visima vya vijiji vingine vilivyosalia. Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetangaza zabuni tarehe 5 mwezi huu wa Aprili, ambapo itachukua miezi minne kukamilisha ujenzi tangu mkandarasi atakapopatikana. Ni matarajio yangu kuwa hadi kufikia mwezi Oktoba mwaka huu wa 2012, miradi hiyo itakuwa imekamilika.

MHE. MARIA I. HEWA: Ahsante Mheshimiwa Spika. Naomba niulize swali moja tu la nyongeza. Miradi hii inayofadhiliwa na Benki ya Dunia inasuasua sana na mingi imeshindikana kabisa. Je, Serikali inaweza sasa kulibebea bango suala hili la miradi hii ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa kuingilia kati ili miradi hii iweze kukamilika? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nitoe ufanuzi kwamba tunavyosema miradi ya Benki ya Dunia, siyo sawasawa. Tunasema Benki ya Dunia ni mojawapo ya washirika wa maendeleo katika kutekeleza programu nzima ya maji. Sasa si mradi wa Benki ya Dunia kwa sababu katika Mfuko wa Pamoja, Serikali imeweka fedha zake na washirika wengine. Kwa hiyo, tunaweza tukasema kipengele fulani katika mradi fulani kwenye Halmashauri fulani unasuasua, si katika mradi mzima kama ulivyo. Kwa hiyo, naomba nitoe ufanuzi huo, ni kwamba katika hatua za utekelezaji kuna miradi ambayo tunasema ni *earmark projects*, wafadhili wameenda moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi na miradi mbingi imeenda vizuri, mpaka sasa hivi maji yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya vijiji 10, sasa hivi Halmashauri 106 tayari wameshapata wakandarasi wa kuanza kujenga miundombinu. Kwa hiyo, ni hatua nzuri ambayo nina hakika kabisa na nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuwe na imani kwamba mradi huu unatekelezeka na baada ya muda si mrefu tutaanza sasa kutoa kwenye tenki baada ya wakandarasi wale kumaliza kazi zao.

Na. 9

Ubinafsishaji na faida zake kwa Taifa

MHE. AMINA M. MWIDAU (K.n.y. MHE. MAGDALENA H. SAKAYA) aliuliza:-

- (a) Je, Watanzania wamenufaikaje na ubinafsishaji uliokwishafanyika?
- (b) Kwa sababu viwanda vingi vilijengwa kimkakati kuendana na mahitaji ya wananchi na malighafi zinazopatikana kwenye maeneo husika, je, Serikali inasema nini juu ya kubadilishwa kwa matumizi ya viwanda hivyo tofauti na makubaliano ya mkataba wa kubinafsishwa?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mbunge (Viti Maalum), lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, baada ya ubinafsishaji, mashirika mengi yamefuliwa na hivyo yameweza kutimiza malengo ya kuongeza tija kwa Watanzania kama ifuatavyo:-
- (i) Ubinafsishaji umeimarisha na kuongeza uzalishaji, viwanda vilivyokuwa vimesitisha uzalishaji vimefuliwa na kuongeza uzalishaji na kuimariswa pale ambapo ulikuwa ukisusua. Uzalishaji huu umeongeza bidhaa kwenye soko la ndani na hata mauzo ya nje. Vilevile uzalishaji huu umeokoa mahitaji ya fedha za kigeni ambazo zingetumika kuingiza bidhaa hizo. Vilevile kuongeza fedha za kigeni pale bidhaa hizo zilipouzwa nje na kuongeza thamani ya mazao ya ndani hasa ya kilimo.
 - (ii) Ubinafsishaji umeongeza fursa za ajira na mapato na hivyo kupunguza umaskini wa kipato na kuchochea ukuaji wa uchumi. Aidha, uzalishaji na ajira kwa pamoja vimeongeza mapato ya Serikali kuitia kodi mbalimbali na hivyo kuimariswa utoaji wa huduma kwa Watanzania yaani jamii.
 - (iii) Ubinafsishaji umesaidia uhamishaji wa teknolojia na uzalishaji wa sasa unafanyika kwa ufanisi zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Aidha, Watanzania wengi wameongeza weledi (*skills*) katika uzalishaji wa kisasa kuitia Taasisi zilizobinafsishwa.
- (b) Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na hoja ya Mheshimiwa Sakaya kwamba kumekuwa na wakati na kubadilishwa kwa matumizi ya baadhi ya viwanda tofauti na makubaliano ya mikataba baada ya kubinafsishwa. Hata hivyo, Serikali imewaruhusu baadhi tu ya wawekezaji kubadili matumizi ya viwanda pale ambapo mabadiliko hayo yameonekana kuwa na manufaa zaidi kwa Taifa na Watanzania. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali iko makini katika kusimamia na kufuatilia viwanda na mashirika yaliyobinafsishwa ili kuona malengo na madhumuni ya ubinafsishaji huo yanatimizwa ipasavyo.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mepesi kidogo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ukilinganisha na uzito wa swali lenyewe, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake la msingi amesema kuwa baada ya ubinafsishaji mashirika mengi yamefulufiwa na kwa kuwa swali hili ni la kuandika na amekaa nalo muda mrefu, nina imani ana takwimu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akatupatia idadi ya mashirika ambayo yamefulufiwa na ambayo hayajafufuliwa na kwa nini? (*Makofi*)

Pili, kwa taarifa kwa takwimu ninazozifahamu, nchi yetu Tanzania tunaagiza zaidi kutoka nje kuliko kuuza katika soko la nje na katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa ubinafsishaji umesaidia kuongeza uuzaaji wa bidhaa katika soko la nje. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akatupatia takwimu ni kwa kiasi gani baada ya ubinafsishaji tunauza katika soko la nje kuliko ku-*Import* kutoka nje ya nchi? Ahsante.

SPIKA: Swali lako lingekuwa zuri sana kama lingekuwa fupi, maana sasa umechanganya mambo mengi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu na utumie muda mfupi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Spika, mwaka 1993 jumla ya mashirika 78 yalikuwa yamesitisha uzalishaji kabisa na yakabinafsishwa. Kwa taarifa niliyonayo kama mashirika 42 yamefulufiwa na yanafanya kazi. Kuna mashirika ambayo yanasuasua na mengine hayakuendelezwa kama 17 ambayo tunayafuatilia na kuwasiliana na wahusika na ikiwezekana tuyahamishe kwenye umiliki wao.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu takwimu za *import* na *export*, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli bado tuna nakisi katika *imports* na *exports* zetu lakini kwa kiasi kikubwa *imports* zetu ni za *capital goods* au bidhaa za uzalishaji na nakisi imeendelea kupungua. Sina takwimu sahihi kwa sasa lakini namuahidi kumpatia baadaye.

SPIKA: Unadaiwa na zingine nilishakuagiza ulete siku nyingi lakini mpaka leo hujaleta, ilikuwa ni kuhusu wale walioopata ruzuku kwa ajili ya kupandisha thamani ya fedha. Mheshimiwa Zitto swali lingine.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa na majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa kuhusiana na mafanikio au kutofanikiwa kwa ubinafsishaji. Napenda kumwuliza kama kuna mafanikio kwenye ubinafsishaji, inakuwaje mwaka 1980 tulikuwa tuna viwanda 12 vya korosho vilivyokuwa vinafanya kazi leo ni kiwanda kimoja tu kinafanya kazi. Kama tumefanikiwa katika ubinafsishaji iko wapi *Mwanza Textile (MWATEX)*? Iko wapi *Mbeya Tex*? Iko wapi *Sungura Tex*?

Viko wapi viwanda vya nguo ambavyo waasisi wa nchi hii walivianzisha kwa ajili ya kukuza ajira na kukuza uchumi wa nchi hii? Leo Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaweza akasimama na kusema kwamba ubinafsishaji una mafanikio katika nchi hii? (*Makof*)

SPIKA: Siyo Naibu Waziri tu anaweza kujibu hata wewe Waziri unaweza kujibu. Mheshimiwa Waziri hebu ulijibu swali hili. (*Makof*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Naibu Waziri kwamba amejibu kwa jinsi swali liliyoulizwa. Kwa hiyo, yale yaliyoulizwa ameyajibu sawasawa. Sasa kama kuna mengine *specific* ya viwanda vya *Textile* na viwanda vingine, hayo nadhani Mheshimiwa atuletee swali rasmi na tutalijibu rasmi kwenye *statistics*.

SPIKA: Hapana, hayo siyo majibu Mheshimiwa Waziri. Wanachouliza mafanikio ya ubinafsishaji, hiyo ni mifano, mimi nilitegemea ninyi mtajibu mifano. Kwa hiyo, hili jibu bado hamjajibu. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini. (*Makof*)

Na. 10

Kusambaza umeme Jimbo la Kyerwa

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alipofanya ziara katika Jimbo la Kyerwa aliwaahidi wananchi wa Jimbo hilo kuwa watafikishiwa umeme kwenye vijiji vyao:-

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mbunge wa Kyerwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vijiji vya Kyerwa yanategemea kupata umeme chini ya mpango unaosimamiwa na Serikali ya Tanzania na Uganda wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa nguvu za maji eneo la Murongo/Kikagati kutoka Mto Kagera. Kulingana na tathmini ya upelekaji umeme katika vijiji vya Jimbo la Kyerwa iliyofanyika mwaka 2009, gharama za upelekaji wa umeme katika Jimbo la Kyerwa utagharimu shilingi billioni 20.3. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa 33kv yenye urefu wa kilomita 194.5 na uwekezaji wa transfoma 49.

Mheshimiwa Spika, kituo cha kufua umeme cha Murongo/Kikagati kinatarajiwa kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme megawati 16 ambapo Uganda watapata megawati nane (8) na Tanzania tutachukua megawati nane (8). Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2012, baada ya kukamilika kwa majadiliano baina ya wataalamu wa nchi hizi mbili na mkandarasi. Mazungumzo hayo yamefika kwenye hatua nzuri na yanashubiri kuafikiwa na Mawaziri wa Nishati wa Tanzania na Uganda.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri na ya kutia matumaini, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Kyerwa sasa ni Wilaya mpya na kwa kuwa kutakuwa na Makao Makuu ambayo sasa hivi hayana umeme na kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri itachukua muda ili kuweza kupata umeme kutokana na mradi mkubwa wa umeme ambao utaanzia Murongo, je, Serikali imeweka mipango gani ya kuweza kutupatia umeme katika Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Kyerwa wakati tunashubiri umeme kutokana na mradi mkubwa ambao ameutaja?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa tulizopata kutoka Kyerwa wamekubaliana kwamba Ruberwa ndiyo patakuwa Makao Makuu ya Wilaya. Kwa sasa hivi kuna mradi wa *REA* ambapo umeme unatoka kwenye kituo kile cha Kayanga-Umurushanga kwenda Nyakasana utakwenda mpaka Rwabele. Nadhani mradi huo unatekelezwa na *REA* na uko Jimboni kwa Mheshimiwa Blandes. Sasa tunachoweza kufanya ni kwamba kutokea pale Rwabele mpaka Rubelwa pana kama kilomita 20 au 25 hivi, wakati tunashubiri mradi wa Murongo/Kikagati ukamilike ambao unaweza ukachukua kama miezi 30 hivi tangu mwezi Oktoba, katika kipindi hiki nitashauriana na wenzangu Wizarani pamoja na *REA* na *TANESCO* ili tuone utaratibu wa kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya Ruberwa kutoka kituo cha Rwabele ambacho ni kama kilomita 20 lakini pia tutaangalia *technical details* kama umeme unaofika Rwabele utatosha kuongeza hizo kilomita 20 kwenda mpaka Makao Makuu ya Wilaya.

Na. 11

Kupeleka Umeme Kituo cha Afya cha Puge

MHE. SHAFFIN A. SUMAR aliuliza:-

Wilaya ya Uyui haina hospitali ya Wilaya lakini kuna kituo cha Afya cha Puge ambacho kinahudumia wakazi wengi wa Wilaya na kituo hicho hakina umeme licha ya kuwa kipo umbali wa kilomita saba kutoka kwenye nyaya za *TANESCO*:

Je, Serikali haioni umuhimu kukipatia umeme kituo hicho ili kuongeza ubora wa huduma inayotolewa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini ya gharama ya kipande hiki cha mradi yaani ili kufikisha umeme katika kituo cha Afya cha Puge inakadiriwa kufikia shilingi za Kitanzania milioni 320. Gharama hizo ni kwa ajili ya kujenga njia kuu ya msongo wa kilovoti 33 umbali wa kilomita tisa, ujenzi wa kilomita moja ya njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 *line, distribution line*, pamoja na ufungaji wa kipooza umeme (transfoma) chenye nguvu ya *kVA* 100; 33/0.4*kV* kwenda kwa wateja mbalimbali wanaokisiwa kufikia 46, mashine za unga kama tatu na kituo kimoja cha kusukuma maji ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, suala la kupeleka umeme katika Jimbo la Tabora Kaskazini limeshatolewa maelezo na Serikali hapa Bungeni, ambapo Serikali ilitoa ahadi ya kupeleka umeme kwenye maeneo ya Ndala na Puge. Serikali inatambua umuhimu wa kituo cha afya cha Puge ambacho ndicho kinachohudumia wakazi karibu wote wa Wilaya ya Uyui kutohana na kutokuwepo kwa Hospitali ya Wilaya.

Serikali kuititia Shirika la Umeme *TANESCO* na *REA* imechukua jitihada za makusudi kuhakikisha fedha kwa ajili ya ufadhilli wa mradi huu zinapatikana katika mwaka wa fedha 2012/2013, ili mradi huo uweze kukamilika na huduma muhimu kuwafikia wananchi.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini kuna maeneo mawili ameyataja ambayo ni Ndala na Puge, nataka niseme kwamba, maeneo haya mawili hayamo kwenye Jimbo langu la Tabora Kaskazini, Wilaya ya Uyui yamo Wilaya ya Nzega. Sisi tuna kituo cha Afya kimoja tu cha Ukuge ambacho hakina umeme, lakini pia tuna shule nyingi za sekondari na zahanati nyingi ambazo umeme unapita lakini huduma haijapelekwa pale, nini mpango wa Serikali kuhusiana na maeneo hayo? (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, umejibu maeneo siyo ya kwake.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nilichosema ni kwamba, hapa tulipokuja kama miezi kumi na nane iliyopita tuliposema tutapeleka umeme kwenye maeneo ya Ndala na Puge ilikuwa ni mradi mkubwa ambao hii programu ya kupeleka kwenye kituo cha afya ilikuwa ni sehemu ya mradi huo. Sasa kwa sababu ya matatizo yaliyotokea hapo katikati na mradi huo ukashindwa kutekelezeka, ndiyo tukasema kipande hiki tumekipatia umuhimu wa kipekee kwa sababu ya hiki kituo cha afya ambacho kinakidhi mahitaji ya wakazi wote pale. Kwa hiyo, kwa ujumla, upana wa mradi ule bado unaendelea, lakini kwa sasa hivi *specifically* tunataka kukamilisha hili la kituo cha afya kwa sababu ya kukosekana kwa hospitali ya Wilaya katika eneo hilo.

SPIKA: Ahsante. Sasa tunakwenda Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Lekule Laizer atauliza, kwa niaba yake, nyie wote, kwa niaba yake hakuna? Mheshimiwa Mangungu, kwa niaba yake.

Na. 12

WMA Kuwezesha na Kukusanya Mapato ya Utalii

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. MICHAEL L. LAIZER) aliuliza:-

Maeneo mbalimbali yameanzisha *WMA* lakini mpaka sasa bado hawawezi kukusanya mapato na kazi hiyo bado inafanywa na *CITES* huku wananchi hawajui lolote licha ya kwamba *WMA* inapewa asilimia 65 ya mapato:-

- (a) Je, ni lini *CITES* itawaachia wananchi kukusanya mapato yao kama utaratibu unavyoeleza?
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuwaondoa wawekezaji kwenye eneo la *WMA* ambao hawataki kuondoka wala kukutana na uongozi wa *WMA*?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, swali lako refu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido lenye sehemu (a) na (b) naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa *WMA* zimeshaanzishwa katika maeneo mengi nchini. Baadhi ya *WMA* hizo zimeanzishwa katika maeneo ya vijiji ambayo yalikuwa na vitalu vya uwindaji vilivyokuwa na mikataba kati ya Serikali na kampuni za uwindaji. Kufuatia kuanzishwa kwa *WMA* hizo, maeneo hayo yanahitaji kusimamiwa na wananchi na kukusanya mapato kutokana na rasilimali zilizoko kwenye maeneo hayo. Baadhi ya maeneo yaliyoanzisha *WMA* yalikuwa chini ya vijiji ambavyo villingia mikataba kati ya wawekezaji na vijiji husika kabla ya *WMA* kuanzishwa na kutangazwa.

Mwaka 2009, Wizara ilikubali maombi ya wananchi kwamba isimamie kukusanya mapato katika maeneo ya *WMA* wakati *WMA* hizo zikijjengewa uwezo wa kukusanya na kusimamia mapato.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya kuwepo kwa malalamiko kuwa:-

- (1) Mapato waliyokuwa wakilipwa wananchi kutoka kwa wawekezaji yalikuwa kidogo;
- (2) Baadhi ya kampuni zilikuwa hazilipi ilivyostahili ikilinganishwa na mapato yao;
- (3) Mapato kidogo yaliyokusanywa yalikuwa yakiwanufaisha wananchi wachache, hasa viongozi;
- (4) *WMAs* zilikuwa hajijajengewa uwezo wa kukusanya na kusimamia mapato yanayojumuisha mapato ya Serikali kutoka kwenye maeneo yao; na
- (5) Kutokuwepo kwa utaratibu au kanuni za usimamizi wa kukusanya mapato kutoka kwa wawekezaji hasa maeneo ya utalii wa picha.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2009 hadi Disemba 2011, jumla ya US\$816,962.92 sawa na shilingi 1,225,444,380 zilikusanywa katika maeneo mbalimbali yanayoendesha utalii wa picha katika Wilaya za Serengeti na Longido. Kati ya fedha hizo, *WMA* ya *Endowment* ilipata jumla ya US\$143,005.25 yaani sawa na shilingi 214,507,875.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa kuzingatia kuwa kuna wadau wengine kwenye maeneo ya *WMA* wanaostahili kunufaika, mgawanyo wa mapato unazingatia shughuli muhimu kama ifuatavyo:-
- (1) Utalii wa picha- *WMA* zinapata mgao wa asilimia 65, Halmashauri za Wilaya 15% na Wizara 20%.
- (2) Uwindaji wa kitalii unaofanyika kwenye *WMAs* - *WMA* zinapata 25% ya ada za wanyama waliowindwa kwenye maeneo hayo; mfuko wa kuhifadhi wanyamapori (*TWP*) 25%, Wizara 30% na Halmashauri za Wilaya 15%.
- (b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na wafadhili, inaendelea kutoa mafunzo kwa wataalam walioko karibu na maeneo ya *WMA*. Mafunzo hayo hutolewa kwa wataalam ili waweze kuwajengea uwezo wananchi kuhusu kuanzisha, kusimamia na kukusanya mapato kwenye *WMAs*. Baada ya kukamilika kwa mafunzo hayo na kuthibitisha kujengeka kwa uwezo, wananchi wataruhusiwa kuanza kukusanya na kusimamia mapato.

Mheshimiwa Spika, kampuni inayowekeza kwenye *WMA* ambayo haitaki kuingia mkataba na *WMA* haina budi kuondolewa kwa mujibu wa sheria kwani mwekezaji wa aina hiyo anakiuka kanuni kwenye eneo hilo. Jumuiya za Jamii Zilizoidhinishwa (*Authorized Associations*) zinazosimamia *WMA* husika zinayo mamlaka ya kuchukua hatua za kisheria. Katika kutekeleza hilo, Wizara yangu itashirikiana na (*Authorized Associations*) ili kuhakikisha wawekezaji wasiokuwa na mikataba halali wanachukuliwa hatua stahili za kisheria.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri, lakini ningependa nimuulize maswali kadhaa ya nyongeza. Katika majibu yake amesema kwamba, wanatoa utaalam katika jamii na maeneo husika, lakini utaalam huu unatolewa kwa watu wachache sana na vilevile zoezi linachukua muda mrefu sana. Tatizo hili

pamoja na Longido lipo pia katika eneo la Miguruwe, Kandalale na Njinjo katika Jimbo la Kilwa Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ugawaji wa mapato yanayotokana na maliasili limekuwa sugu sana na ni la muda mrefu. Je, ni lini Serikali itakuwa tayari sasa kukaa na viongozi na wadau wa maeneo ya jamii zinazozunguka katika maeneo haya ili kuweza kulimaliza tatizo hili ili lipotee kabisa?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa tukitoa mafunzo kwa wataalam wachache na kama alivyosema wakati mwingine muda unakuwa mrefu, tatizo kubwa kwa kweli ni fedha, upatikanaji wake na kiasi cha fedha kinachopatikana kwa ajili ya shughuli hii.

Wizara kwa kulijua hili tunaongeza jithada za kuongeza ukusanyaji wa mapato na uwezo utakavyokuwa unaimarika tutaweza kuwafikia wengi na kwa muda mfupi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugawanyaji wa mapato kwamba kuna maeneo mengi ambayo yamekuwa hayapati mapato ya kuridhisha, kuna mambo mawili yanafanyika kuhusu jambo hili: Kwanza, tunahimiza sana maeneo ambayo yanazunguka hifadhi kuanzisha *WMA* au hifadhi za jamii za wanyamapor. Kwa kufanya hivyo jamii zitanufaika moja kwa moja na mapato yanayopatikana kutokana na uwindaji au uvunaji wa rasilimali za wanyamapor kwenye maeneo hayo.

La pili, kuna mgao wa asilimia 25 ambaao unarudi kwenye Halmashauri kutoka Hazina baada ya uwindaji kufanyika, kumekuwa na malalamiko kwamba fedha hizi zimekuwa zikichelewa. Tumekuwa na mazungumzo na mawasiliano ya muda mrefu kidogo sasa na wenzetu wa Hazina kwamba ikiwezekana mapato yale tuwe tunaya-*retain* moja kwa moja baada ya uwindaji badala ya kupeleka Hazina halafu yarudishwe kwenye vijiji. Kwa kufanya hivyo, manung'uniko ambayo yamekuwepo yataweza kwisha. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge mwenzangu awe na subira kidogo ili mchakato huu unaoendelea uweze kukamilika na wawahamashe wananchi waweze kuanzisha *WMA*.

Na. 13

Wanafunzi Kufungiwa Kufanya Mitihani

MHE. YAHYA KASSIM ISSA aliuliza:-

Serikali ilitoa kauli kuwa wanafunzi waliofanya udanganyifu katika mtihani wa kidato cha nne 2011 hawataruhusiwa kufanya mtihani kwa kipindi cha miaka mitatu:-

- (a) Je, uamuzi huo umefanywa kwa mantiki gani na faida gani kwa Taifa?
- (b) Je, Serikali haikuona adhabu nyingine ya kuwapa wanafunzi hao na kuamua adhabu hiyo inayowanyima haki ya kusoma na kutahiniwa?
- (c) Je, Serikali inaweza kueleza ni kwa namna gani mitihani inavunja na kumfikia mwanafunzi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ilitoa kauli kuwa watahiniwa waliofanya udanganyifu katika mtihani wa kidato cha nne uliofanyika Oktoba, 2011 hawataruhusiwa kufanya mitihani kwa kipindi cha miaka mitatu. Uamuzi huo umefanywa kwa kuzingatia ongezeko la vitendo vya udanganyifu katika mitihani ukiwa na lengo la kukomesha vitendo hivyo ambavyo vinarudisha nyuma juhudzi za Serikali za kutoa elimu bora kwa wote.

Hivyo, kutoruhusu watahiniwa wanaofanya udanganyifu kwa miaka mitatu ni adhabu iliyotolewa kwa lengo la kuonesha kuwa udanganyifu katika mitihani ni suala lisilokubalika kabisa na kuwafanya watahiniwa watarajiwa kuwa makini zaidi katika kuzingatia taratibu za uendeshaji mitihani. Aidha, uamuzi huo umefanyika kwa mujibu wa kifungu 6(2)(b) cha kanuni za mitihani kinachosomeka, "*a candidate who found to have committed an examination offence shall be excluded from all future examinations set by the council*"

Hata hivyo, Serikali imeona iware nafasi tena watahiniwa husika kufanya mitihani hiyo baada ya miaka mitatu.

Hatua hii inalisaidia Taifa kudhibiti viwango vya ubora wa yeti vya elimu kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi.

- (b) Mheshimiwa Spika, adhabu inayotolewa kwa watahiniwa waliofanya udanganyifu katika mtihani hutokana na Kanuni za Mitihani. Kifungu cha 6(2)(a)(b)(c) cha kanuni za Baraza la Mitihani. Hivyo, adhabu waliyopewa watahiniwa ya kutofanya mitihani kwa kipindi cha miaka mitatu haiwanyimi fursa ya kusoma kwani wanaweza kuanza maandalizi kuanzia sasa kama watahiniwa wa kujitegemea ili baada ya miaka mitatu waweze kufanya mitihani yao kwa kujiamini zaidi. Aidha, watahiniwa hawajanyimwa haki yao ya kutahiniwa kwa kuwa baada ya miaka mitatu wanaweza kujisajili kama watahiniwa wa kujitegemea (*Private candidates*) yaani wanafunzi wa kujitegemea.
- (c) Mheshimiwa Spika, kuhusu namna ambavyo mitihani huvuja na kuwafikia wanafunzi, napenda kueleza kuwa maana ya neno kuvuja kwa mtihani ni watahiniwa kupata maswali kabla ya mitihani kufanyika. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı haikupokea taarifa yoyote ya kuvuja mtihani wa kidato cha nne 2011 kwa kipindi chote ambapo mtihani huo ulikuwa ukifanyika. Kilichojitokeza ni udanganyifu katika mitihani ambapo wakati wa usahihishaji ndipo ilipobainika kuwa baadhi ya watahiniwa walikuwa na miandiko tofauti kwenye skripti zao, wengine kuingia kwenye chumba cha mtihani na simu na wengine kuwa na majibu ya mfanano usio wa kawaida. Jambo linaloonesha kuwa zaidi ya mtu mmoja alishiriki kumwandikia mwenzake majibu. Aidha, baadhi ya watahiniwa walikamatwa wakiwa na *notes* ndani ya chumba cha mtihani na wengine walibainika kuwa na majibu hayo mfanano usio wa kawaida. Hivyo, kilichotokeza ni udanganyifu katika mtihani wakati inaendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwaasa watahiniwa wote na wazazi na watahiniwa watarajiwa wa mwaka huu kuhakikisha wanazingatia kikamilifu sheria za Baraza la Mitihani ili kuepuka udanganyifu.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa darasa la saba waliofanya udanganyifu wameruhusiwa kufanya mtihani mwaka

huu, kuna tofauti gani hawa *form four* wamewekewa miaka mitatu na wote wamefanya udanganyifu wa mtihani? (*Makofii*)

Kwa kuwa katika mtihani wako wanaotunga mtihani, wako wanaochapa mitihani, wako wanaokusanya mitihani, wako walimu wanaosimamia mitihani na ukiangalia wanafunzi ni sehemu ya mwisho. Je, hawa wote waliokuwa wametangulia na tunajua kwamba mwanafunzi hawezi kupata mtihani isipokuwa kutokana na watu hawa...

SPIKA: Sasa uliza swali usituhutubie.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Hawa wamepewa adhabu gani?

SPIKA: Waziri majibu mafupi na ya kwenu yalikuwa marefu.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba mitihani haikuju na nimesema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haikuwa na taarifa kabla ila ilianza kupata taarifa wakati wa usahihishaji. Kwa hiyo, ilikuwa ni vigumu kusema kwamba, mitihani ilivuja pale Baraza la Mitihani au huko ilikokuwa inasafirishwa. Lakini kilichojitokeza kutokana na ufuatiliaji uchunguzi ni kwamba, kama nilivyosema mitihani ilipofika kwenye vituo, wasimamizi na walimu kwa baadhi ya shule walihusika na udanganyifu huu na hatua kali zitachukuliwa dhidi yao kama ambavyo tayari tumeshaanza kuchukua hatua kwa mitihani ile ya darasa la saba. Tarehe 15 Machi, tumemaliza kuwawajibisha waliokuwa wamefanya udanganyifu kwenye mitihani ya darasa la saba tunaingia sasa kwenye uchunguzi maalum kwa ajili ya mitihani ya kidato cha nne. Kwa hiyo, naomba tuwe wavumilivu, tutaleta ripoti maalum kwamba walimu waliokuwa wamehusika pamoja na wasimamizi ni hawa hapa na hatua stahiki za Serikali zitachukuliwa.

Na. 14

Kituo cha Polisi Ifunda Kuwepo Ndani ya Nyumba ya Mtu Binafsi

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA aliuliza:-

Kituo cha Polisi Ifunda (Wilaya ya Iringa) kiko katika nyumba ya mtu binafsi na hakina hata gari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta jengo pamoja na gari kwa ajili ya kituo hicho kinachuhudumia Kata za Ifunda, Limuli, Maboga na Wasa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dokta William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo cha polisi Ifunda hakiko katika nyumba ya mtu binafsi, majengo ya kituo hicho pamoja na jengo la Mahakama ya Mwanzo Ifunda ni mali ya Serikali kwani yanamilikiwa na wakala wa majengo (*TBA*). Hata hivyo, Serikali inaendelea na mpango wa kujenga vituo vya polisi katika Kata zote nchini zikiwemo alizozitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kituo cha polisi Ifunda hakina gari, lakini kimepewa pikipiki moja na pale ambapo inabidi magari yaliyopo Wilayani na Mkoani hutumika.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya ufanuzi, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, wananchi wa Tarafa ya Kiponzerwa ambapo kituo hicho kipo Ifunda, kwa kufahamu kuwa wana tatizo kubwa na huduma hii na Polisi, wao wenyewe sasa wameamua kuchangia matofali pamoja na mawe ili kuhakikisha kwamba kuna kituo cha Polisi kwa kuwa nyumba ile ni chumba kimoja pamoja na sebule, hakikidhi hata kidogo sifa ya kituo cha Polisi wala huduma inayohitajika. Je, Serikali iko tayari sasa kuungana na wananchi pamoja na ufinyu wa bajeti kutenga fungu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaunga mkono ujenzi wa kituo hicho kimalizike kama wananchi tulivoamua?

Pili, ni kweli kituo hicho wamepewa pikipiki, lakini pikipiki kwa kutembelea vijiji 30 kwa sababu tuna Kata nne pamoja na vijiji vinne vya Kata ya Mgama kwa hiyo Askari wanasumbuka sana kuhudumia mpaka vijiji 30, haikidhi hata kidogo huduma ya pikipiki. Ni kweli inapobidi na wakati tunapofanikiwa kupata gari kutoka Wilayani huwa wanahudumiwa, lakini kwa kuwa kazi ni kubwa na mahitaji ya gari bado ni makubwa sana. Je, Waziri anaungana na mimi kwamba, sasa ni wakati tunapoelekea kwenye bajeti kutenga angalau bajeti ili kituo kile kiwe na gari la kuhudumia wananchi hao wanaohangaika kwa kuhudumiwa na kituo kidogo kisicho na usafiri?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, niseme kwamba nimezipokea hizo taarifa za wananchi wa Tarafa ya

Ifunda katika jitihada zao za kujenga kituo na jitihada ambazo zinafanyika katika maeneo mbalimbali ya Taifa letu na hii inaonesha umuhimu ambao wananchi wanaweka katika ulinzi na usalama wao.

Niseme kwamba hili tutalitazama Mheshimiwa Mbunge kwa sababu madai ni mengi, lakini tatizo tulilokuwa nalo na nataka niliseme bila kificho chochote ni ufinyu wa bajeti, ni hali ya fedha ambayo tulikuwa nayo na ningependa kutangaza hapa katika Bunge lako Mheshimiwa Spika kwamba, Serikali iko tayari na Wizara iko tayari, lakini tatizo kubwa ambalo tunalo ni tatizo la kifedha. Hata hivyo, mchango huu wa wananchi ningependa tuzungumze zaidi na Mheshimiwa Mbunge na hata ikibidi baadhi ya uongozi pale tuone ni jinsi gani tunaweza tukafanya, lakini niseme kwamba jitihada ni nzuri.

Kuhusu suala la pili la vitendea kazi na hapa tunazungumzia pipipiki ambayo ipo katika kituo hicho, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili ni tatizo ambalo linakabili si eneo lake peke yake lakini Wabunge wengi waliokuwepo hapa ndani ya jengo hili, hili ni tatizo ambalo limekuwa linatukabili na Wizara imekuwa inafanya kila jitihada na niseme tutaendelea kufanya jitihada. Lakini pia Wabunge mnajua bajeti inapitia mikononi mwenu, mnaitazama ninyi wenyewe lakini tatizo kubwa tulilonalo ni taratibu za kifedha lakini pale ambapo itaruhusu na itakapokuja katika mtazamo wa bajeti hii inayokuja tutatazama ni maeneo gani ambayo tutaweza kuweka vitendea kazi ikiwa ni pamoja na eneo hili ambalo amelitaja Mheshimiwa Mbunge, lakini niseme kwamba yote itategemea na hali ya fedha itakayokuwepo.

SPIKA: Haya, ukishakuwa huna hela maneno yanakuwa mengi. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata Wizara ya Habari, Vijana na Michezo Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia atauliza swali hilo. Mheshimiwa Juma Nkamia hayupo? Basi Mheshimiwa Simbachawene!

Na. 15

Kuboresha Majengo TBC

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (K.n.y. MHE. JUMA S. NKAMIA) aliuliza:-

Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) ni muhimu kwa Taifa na limetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza na kuboresha majengo ya Shirika hilo ambayo yapo katika hali mbaya?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
(K.n.y. NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO)**
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua nafasi hii kumpa pole sana Mheshimiwa Waziri wa Habari na Utamaduni kwa kufiwa na Ndugu yetu Steven Kanumba.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya Makao Makuu ya *TBC* yamejengwa miaka zaidi ya 50 iliyopita na kwa muda mrefu hayajafanyiwa ukarabati kutokana na uhaba wa fedha za maendeleo. Aidha, jengo la Studio za televisheni liliopo Mikocheni bado halijakamilika. *TBC* imejaribu kutafuta fedha za kumalizia jengo hilo na kukarabati studio za redio na Makao Makuu kwa kukopa fedha za Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*).

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kulidhamini Shirika la Utangazaji Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo ya Serikali na Udhamini ya Mwaka 1974 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2004 yaani (*The Government Loans, Guarantees and Grants Act, 1974 as amended in 2004*) ili liweze kupata mkopo kutoka Taasisi mbalimbali zinazotoa mikopo. Aidha, mawasiliano yanaendelea kufanyika katika *TBC* na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ili kuona uwezekano wa *TBC* kupata mkopo katika shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za Miradi ya Maendeleo kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wao.

SPIKA: Mheshimiwa Simbachawene swali la nyongeza litakuwa moja tu!

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nitajaribu kuyaweka kwa pamoja. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya *TBC* na matatizo iliyonayo hususan hili la uchakavu wa majengo lakini pia hatia kuwa na *studio* ambazo zimechoka na pia vitendea kazi vilivyochochoka na ukizingatia kwamba suala la habari kwa sasa ni suala ambalo sekta binafsi nayo inashiriki na kwa hiyo *TBC* kama shirika la umma linashindana na vyombo vingine na kazi kubwa ambayo imefanya na *TBC* katika nchi hii ni kazi iliyotukuka.

Serikali haioni haja ya kuchukua hatua za dharura kuhakikisha kwamba inaboresha hata kwa majengo yake mengine ambayo Serikali ya Tanzania ina majengo mengi na mazuri, haiwezi ikasema haina uwezo hata wa kununua kamera, haiwezi kusema haina hata uwezo wa kutengeneza studio inayoweza kushindana na *studio* nyingine kama zilivyo studio za radio nyingine za binafsi.

Mheshimiwa Spika, *this is very serious*, naomba Serikali itoe commitment hapa namna ya ku-rescue situation mbaya ya *TBC*.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa George Simbachawene anatusaidia sana hapa, ni kila mtu anafahamu kabisa kwamba Shirika letu la *TBC* limefanya kazi nzuri sana katika nchi yetu ya Tanzania na kutangaza mambo yote ya utalii na mambo yote tunayofanya Bungeni na maendeleo yote ya nchi yetu na uchumi wa nchi yetu, hakuna mtu yejote ambaye *ata-dispute* hapa akatae aseme kwamba *TBC* haijafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, anachosema hapa sasa anazungumzia kuhusu hili ambalo Mheshimiwa Nkamia amelileta hapa la kusaidia sasa kuona kwamba tunaliondoa Shirika katika hali hii.

Mheshimiwa Spika, wakati nawasiliana na Mkurugenzi, mmoja wa Wakurugenzi anayehusika na jambo hili, nilimuuliza kwamba hii kazi yote anayozungumza Mheshimiwa Nkamia ni kiasi gani? Akaniambia ni bilioni 18. Bajeti ni mpango wa Serikali unaoonesha jinsi fedha zitakavyopatikana na namna zitakavyotumika. Ni kweli kabisa kwamba kila mtu angependa tuingilie kati kwa maana ya Serikali kusaidia Shirika hili liweze kuondoka katika hali hiyo na ndiyo maana katika hili jibu lililotolewa hapa tumezungumza habari ya kwamba sasa tunajaribu kuangalia namna ambavyo tutashirikiana na NSSF ili wasaidie kutoa fedha hizo kwa utaratibu ule ambao unafanyika katika vyombo vingine ili tuweze kuondoka katika tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Simbachawene kwamba kuna haja ya kuingilia kati kwa maana ya *intervention* ili tuondoke hapo. Kwa hiyo sasa, sisi tutakachofanya, tutamshauri Waziri hili jambo limeanza na Mheshimiwa Juma Nkamia mwenyewe ndiye anaye-*advocate* jambo hili na kusema kwamba kuna haja ya kuona mashirika haya yanasaki. Tutafanya hivyo na kama alivyosema Mheshimiwa George Simbachawene, tutam-*advice* na kumshauri Waziri ili aone kwa namna gani hasa kwa kuzingatia hicho kiasi cha fedha kinachohitajika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na tumeongeza muda zaidi ya ule unaostahili ingawa tumechukua kwa sababu tulikuwa na shughuli kabla ya maswali lakini tumeongeza zaidi.

Naomba niweke suala moja wazi hapa, kwa mujibu wa kanuni ya 45(3) swali la tisa liliopaswa kujibiwa na Wizara ya Fedha nilisema halikupata majibu na kanuni hiyo inasema hivi:-

"Iwapo Spika ataridhika kuwa swalii la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha, ataagiza ijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge"

Kwa hiyo, swalii namba tisa (9) pamoja na swalii la nyongeza aliloulizwa litapewa majibu tena na tutalipanga katika kipindi hiki.

Naomba nitangaze wageni tulionao hapa nao ni Wageni wa Waziri wa Wizara ya Kazi na Ajira, Mheshimiwa Kabaka kutoka shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi yaani *TUCTA*. Hawa ni Ndugu Nicholaus Mgaya, Katibu Mkuu *TUCTA*, sijui yuko wapi lakini asimame alipo. Ahsante, karibu sana. (*Makofii*)

Pia yupo na Ndugu Ezekiel Olochi na yeye asimame alipo. Ahsante sana. Pia tuna Ndugu Brigita Senguaja naye asimame, karibu sana na tunashukuru kwa kuja kututembelea. (*Makofii*)

Pia kuna matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo tarehe 10 Aprili, kutakuwa na kikao cha Kamati saa 7.00 mchana na kitafanyika katika Ukumbi namba 231. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati hiyo wafahamu hivyo.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa anaomba pia niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo hii, haiwezekani baada ya kuahirisha, nadhani saa saba, kikao cha Kamati yake pia kitakaa katika Ukumbi namba 227, nao pia saa 7.00.

Pia tangazo la kwangu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge tutasitisha shughuli za Bunge ili twende kwenye *briefing* ya kawaida, *briefing* zetu huwa tunafanya siku moja kabla ya kikao kama hiki, lakini kama mnavyofahamu tulikuwa na sikukuu na wengi mmefika jana kwa hiyo badala ya kuendelea na kikao cha Bunge kama kawaida sasa hivi saa tano mtakwenda kwenye ukumbi wa Msekwa ili tupewe *briefing* ya

mambo tuliyofanya, halafu baadaye wataendelea na Vyama vyा Siasa baada ya *briefing* yetu yaani mchana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, napenda kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.54 Asubuni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 11 Aprili, 2012 Saa 3.00 Asubuhi)*